

**Swahili B – Higher level – Paper 2**  
**Swahili B – Niveau supérieur – Épreuve 2**  
**Swahili B – Nivel superior – Prueba 2**

Thursday 10 May 2018 (morning)

Jeudi 10 mai 2018 (matin)

Jueves 10 de mayo de 2018 (mañana)

1 h 30 m

---

**Instructions to candidates**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Section A: choose one task. Each task is worth **[25 marks]**.
- Section B: write a personal response to the stimulus provided. The task is worth **[20 marks]**.
- The maximum mark for this examination paper is **[45 marks]**.

**Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Section A : choisissez une tâche. Chaque tâche vaut **[25 points]**.
- Section B : exprimez votre opinion personnelle sur la réflexion fournie. La tâche vaut **[20 points]**.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[45 points]**.

**Instrucciones para los alumnos**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Sección A: elija una tarea. Cada tarea vale **[25 puntos]**.
- Sección B: escriba una opinión personal al estímulo provisto. La tarea vale **[20 puntos]**.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[45 puntos]**.

## Sehemu A

Kamilisha **mojawapo** ya kazi zifuatazo. Andika maneno 250 hadi 400.

### 1. Utofauti wa tamaduni

Mada ya toleo lijalo la gazeti la shule yako ni uwili-lugha. Umepewa jukumu la kuwahoji wanafunzi wenzako ambao wanazungumza lugha mbili kuhusu jinsi uwili-lugha ulivyoimarisha maisha yao katika jamii na kimasomo. Andika mahojiano baina yako na wanafunzi uliowahoji.

### 2. Mila na desturi

Una wasiwasi kuwa nyimbo za kitamaduni zinaendelea kuwa nadra na huenda zikatoweka kabisa hatua isipochukuliwa. Andika pendekezo kwa serikali za mitaa ukieleza ni hatua gani zinahitaji kuchukuliwa kufufua na kukuza nyimbo za kitamaduni, na jinsi itakavyosaidia jamii.

### 3. Afya

Umesoma makala ya gazeti la kitaifa yanayoeleza pendekezo la serikali la kufanya huduma za afya ziwe za bure kwa wote, isipokuwa kwa wale wanaovuta sigara. Andika barua kwa mhariri wa gazeti hilo ukitoa maoni yako kuhusu mpango huu.

### 4. Burudani

Hivi karibuni ulitazama mchezo wa kuigiza ambao ulikugusa sana na kukufanya ufikirie sana kuhusu mchakato wa kukua kwa mtoto hadi kuwa mtu mzima. Andika mapitio ya mchezo huo katika jarida la shule ambapo unatambuliza mchezo huo na kuupendekeza kwa wengine.

### 5. Sayansi na teknolojia

Shule yako inafikiria kuacha kufundisha kwa njia ya kawaida na kuanza mafundisho yote kupitia mtandaoni. Suala hili litajadiliwa katika mkutano ambapo wanafunzi, walimu na wazazi wamealikwa. Kama mwakilishi wa wanafunzi, umeombwa kutoa utambulizi wa mjadala huo kwa kuwasilisha maoni yako kuunga mkono na kupinga hatua hiyo. Andika hotuba yako.

## Sehemu B

Kulingana na kichocheo kifuatacho, toa jibu lako binafsi na ulithibitisha. Chagua maandiko yoyote uliyoyasoma darasani. Andika maneno kati ya 150 na 250.

6. Ili kufaulu siku hizi, vijana wote lazima wafanye kazi mijini badala ya vijijini.
-